# MWONGOZO WA KUSAHIHISHA.

# FORM 4 PAPER 1

1. Majibu yazingatie yafuatayo.

    a. Kichwa kiwe na tarehe, mahali na wakati panapofanyika mkutano.
    b. Waliohudhuria.
    c. Waliokosa kuhudhuria kwa udhuru.
    d. Waliokosa bila udhuru.
    e. Ajenda.
        - Kusoma na kuthibitisha kwa kumbukumbu ya kwanza
        - Shughuli nyinginezo ziwe kumbukumbu ya mwisho.
        - Ajenda za mkutano wa vijana zijadili:
            - Siasa
            - Dawa za kulevya
            - Ukosefu wa kazi
            - Usalama wa vijana vijijini

2. Manufaa ya muungano wa Afrika Mashariki.

    a. Kuimarisha uchumi nchi husika
    b. Kupanua Soko la bidhaa
    c. Kuimarisha Mawasiliano
    d. Umoja wa jamii
    e. Kuimarisha usalama wa mataifa
    f. Kuimarisha utaifa
    g. Utangamano wa michezo.
    h. Kudumisha uhusiano wa kidplomasia.

3. Ni swali la methali
   Abainishe maana ya methali kisha atungie kisa kinachothibitisha methali hiyo.

    Maana: Jambo lisilokuhusu linakukera kivipi au kwa njia gani?

    - Ni vyema kutoingilia mambo yasiotuhusu na yanayoweza kuleta matatizo kama vile ugomvi au vita kati ya watu wawili.
    - Akitoa kisa kisichooana na methali atakuwa amejitungia swali.

4. Kisa lazima kimalizike kwa maneno haya na kisiongezwe chochote.
    - Kisa kieleze jambo kuu la ajabu. Liwe zuri kupita kiasi au baya asana.
    - Kisa kioane barabara na dhamiri na maudhui yaliyokusudiwa
    - Kisa kiweze kumwacha msemaji na mvuto pamoja na taharuki ili kutosheleza kimalizio.